

**CHANGAMOTO ZA USAMBAZAJI DAWA NA VIFAA TIBA MOJA KWA MOJA (DD) KANDA YA DAR-ES-SALAAM**



Barabara ya kuelekea kituo cha afya Msolwa — Stesheni wilayani Kilombelo

Bohari ya dawa (MSD) ilianza kutumia mfumo wa usambazi dawa na vifaa tiba moja kwa moja hadi kwenye vituo vya afya na hospitali (DD) mnamo mwaka 2013.

Mfumo huu ulianza kutumika badala ya mfumo wa awali wa kufikisha dawa na vifaa tiba kwa waganga wakuu wa mikoa na wilaya ambao wao walipeleka kwenye vituo vyao vya afya.

Mfumo wa usambazi dawa na vifaa tiba moja kwa moja hadi kwenye vituo vya afya na hospitali (DD) ulilenga kuondoa changamoto za ucheleweshaji wa usambazaji dawa na vifaa tiba kutoka kwa waganga wakuu.

Katika utekelezaji wake mfumo wa DD umekuwa ukikabiliwa na changamoto mbalimbali hasa kwenye maeneo magumu kufikika.

Dar-es-salaam ni mfano wa kanda inayokabiliwa na changamoto za maeneo magumu kufikika hasa mkoani Morogoro.

Kanda ya Dar-es-salaam inasambaza dawa na vifaa tiba kwenda mikoa ya Dar-es-Salaam, Morogoro na Pwani. Mikoa hii ina vituo vya afya takribani 640, vikiwemo Hospitali, Zahanati na Vituo vya Afya.

Katika utekelezaji wa DD Kanda ya Dar-es-salaam imekuwa ikikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa pamoja na miundo mbinu mibovu hasa ile ya

vituo vya afya vilivyopo vijini pale mvua zinaponyesha kwa wingi.

Kutokana na mvua Barabara nyingi zinakuwa na mashimo na matope ambayo yanasababisha ugumu kwa magari yanayosambaza dawa na vifaa tiba kuvifika vituoni kirahisi.

Mbali na mvua za masika mabadiliko ya tabia nchi, yamekuwa ni changamoto katika usambazaji wa dawa, kwani mvua zinanyesha wakati usiotabirika (bila kufuata misimu ya mvua). Mvua zinaponyesha kwa wingi na huharibu miundo mbinu ikiwemo Barabara, Madaraja, Vivuko n.k.

Katika kipindi cha mwezi Februari 2016 changamoto za miundo mbinu na Tabia nchi zimeshuhudiwa katika maeneo matatu wilayani Malinyi, Ulanga na Kilombelo.

Changamoto ya kwanza ilitokea barabara ya kuelekea kituo cha afya cha Msolwa Stesheni - wilayani Kilombelo mkoa wa Morogoro ambapo gari lililokuwa limebeba dawa kupeleka kituo cha Stesheni lilikwama kwa saa saba (7) kutokana na mvua kubwa iliyonyesha na kuharibu barabara zinazokwenda kwenye kituo hicho.

Dereva (Neemia Zebedayo) alilazimika kuomba msaada kutoka kwa wananchi ili kulikwama gari lilionasa kwenye madimbwi marefu na matope na baadae alifanikiwa kufikisha dawa kwenye

kituo cha Msolwa salama.

Changamoto ya pili ilitokea wakati wa safari ya kuelekea wilaya ya Mahenge na Malinyi. Kwa kawaida safari hii huwa inatumia boti lakini siku hiyo ilishindikana kutokana na mvua kubwa iliyosababisha boti kuzama kutokana na maji mengi.

Kutokana na hali hiyo maderewa wa MSD waliokuwa wanasafiriha dawa walilazimika kuomba msaada wa boti la jeshi kwa ajili ya kuvusha dawa hizo.

Baada ya zoezi la kuvusha dawa kufanikiwa Meneja wa Kanda ya Dar-es-salaam (Sitti Abdulrahman) alilazimika kuwasiliana na Mnga-ga Mkuu wa wilaya ya Ulanga ambapo alipewa gari aina ya land cruiser ambalo lililotumika kusafirishia dawa hizo mpaka vituo vya Afya vya wilaya hizo.

Kwa upande wake dereva (Neemia Zebedayo) amesema imekuwa hali ya kawaida kukutana na changamoto za miundo mbinu pindi wanapopeleka dawa kwenye vituo vya afya nyakati za mvua.



Barabara ya kuelekea Msolwa — Stesheni wilayani Kilombelo



Malinyi - Ulanga



Mto Kilombelo